

UK Health Security Agency

## Kukulinda kutokana na mpox

# Taarifa kuhusu chanjo ya mpox

### Je, chanjo ya mpox (MVA) ni nini?

Unapewa chanjo ili ujisaidie kujilinda dhidi ya mpox. Chanjo ya MVA husaidia kulinda au kupunguza ukali wa maambukiz ya mpox (na Smallpox).


Chanjo hutengenezewa Uropa na Bavarian Nordic. Unapopewa chanjo hiyo, mfumo wako wa kinga mwilini (mfumo wa ulinzi asili wa mwili) hutoa antibodi dhidi ya virusi vya mpox.

Chanjo ya MVA huwa haina virusi vya smallpox au mpox na haiwezi kueneza au kusababisha smallpox au mpox.

Chanjo ya Imvanex imeidhinishwa na Wakala wa Udhibiti wa Bidhaa za Dawa na Afya wa Uingereza (MHRA) ili kutoa ulinzi dhidi ya smallpox na mpox.

Wakala wa Usalama wa Afya wa Uingereza (UKHSA) na Kamati ya Pamoja kuhusiana na Chanjo na Kuchanja (JCVI) inapendekeza matumizi ya chanjo ya MVA kama sehemu ya kukabiliana na visa vya mpox.

**Mpox, (ambayo awali iliitwa monkeypox), ni ugonjwa sugu wa kuambukiza ambao unaweza kujitokeza kama vidonda vyenye uchungu ngozini, vidonda hivi vinaweza kuonekana katika sehemu yoyote ya mwili:**





**www.gov.uk/government/publications/mpox-vaccination-resources**

Mpox GBMSM revised leaflet - Swahili.indd 1 25/02/2025 15:50:08

## Je, mpox ni nini?

Mpox ni ambukizo adimu linalopatikana sana katika Afrika ya Kati na Mashariki.

Ambukizo hili linaweza kusambazwa kutokana na:

- kugusana kwa karibu na matundu au magamba ya mpox (ikiwa ni pamoja na wakati wa ngono, kubusiana, kukumbatiana au kushikana mikono);
- kugusa mavazi, nguo za kitanda au taulo zinazotumiwa na mtu aliye na mpox;
- kugusana na umajimaji wa mwili kama vile mate, kamasi au kohozi.

Kwa kawaida mpox huwa hafifu na unaweza kupungua baada ya majuma machache bila matibabu. Lakini ikiwa dalili zako ni kali zaidi na unaugua, utahitaji matibabu hospitalini.

## Je, MVA inapendekezewa nani?

UKHSA kwa sasa inapendekeza MVA itolewa kwa:

- **Wafanyakazi wa afya ambao wanatunza na ambao wanataka kuanza kutunza wagonjwa ambao tayari wamepatikana na mpox**
- **Mashoga, watu wenye jinsia mbili na wanaume wengine ambao hufanya ngono na wanaume.** Daktari wako atakushauri upate chanjo ikiwa una wapenzi wengi, unashiriki ngono katika makundi au kuhudhuria "ngono katika maeneo"
- **Watu ambao tayari wamekaribiana na mgonjwa aliyethibitishwa kuwa na mpox.** Kuchanjwa kwa kutumia dozi moja ya chanjo kunapaswa kufanywa haraka iwezekanavyo (sanasana ndani ya siku 4 lakini wakati mwingine hadi siku 14)
- **Watu ambao ni wanachama wa kundi au huwa wanahudhuria mazingira ambayo yana kisa kimoja au kundi, au mahali ambapo wanachama wamekaribiana na mtu aliyeambukizwa.**

## Je, chanjo huwa inafanya kazi?

Dozi mbili za chanjo zimeonyesha kutoa kiwango cha juu cha ulinzi dhidi ya mpox. Ulinzi pia huwa mzuri sana baada ya dozi ya kwanza, lakini dozi ya pili wakati mwingine huwa inapendekezwa kwa ulinzi wa muda mrefu.

Chanjo inaweza kukosa kuzuia maambukizi kabisa lakini hata kama utaugua mpox, dalili hazifai kuwa mbaya sana.

Dozi ya kwanza hutayarisha mfumo wa kinga mwilini ili uweze kukabiliana na ambukizo hili kwa haraka zaidi iwapo utakaribiana na mpox.

Pia chanjo huwa inachukua muda kabla ya kufanya kazi. Huenda ikaanza kufanya kazi baada ya siku kadhaa na inapaswa kulinda mtu vizuri kabisa baada ya wiki 4 hivi.

Dozi ya pili inaweza kupeanwa baada ya siku 28 lakini inaweza kupeanwa baadaye, hata baada ya miezi kadhaa. Kuwepo kwa muda mrefu zaidi kati ya dozi ya kwanza na ya pili kunapaswa kuboresha muda mrefu wa ulinzi.

Hata baada ya dozi ya 2 unapaswa kuendelea kujua hatari na dalili za mpox. Iwapo utaanza kuwa na dalili, kaa nyumbani na upige simu kwa 111 au kwa kliniki ya afya ya kingono.

## Je, chanjo hii inaweza kusababisha madhara yoyote?

Chanjo hii ina profaili nzuri sana ya usalama. Kama ilivyo na dawa na chanjo zote, inaweza kusababisha madhara, lakini mengi ya madhara haya huwa hafifu na ya muda mfupi na sio kila mtu huwa anayapata. Kinyume na chanjo ya zamani ya smallpox, chanjo hii huwa haiachi kovu.

Madhara yanaweza kutokea sana kwa watu ambao awali walipokea dozi ya chanjo hai ya smallpox. Watu hawa huwa wanahitaji tu dozi moja ya MVA ili kuongeza ulinzi wao uliopo.

Madhara ya kawaida yanajumuisha maumivu na mwasho kwenye eneo lililodungwa na kuumwa na kichwa, maumivu ya misuli, ugonjwa na uchovu. Mtu mmoja kati ya watu 10 atapatwa na baridi na homa, lakini dalili hizi hazifai kukaa kwa siku nyingi.

Iwapo utakuwa na madhara yoyote yaliyotajwa hapo juu, unapaswa kupumzika na unaweza kumeza dozi sahihi ya paracetamol ili ikusaidie kupunguza dalili hizo.

Ikiwa tayari una ugonjwa wa ngozi wa atopiki (aina fulani ya ugonjwa wa ngozi (eczema)), unaweza kupata dalili kali zaidi za ngozi (kama vile uwekundu, uvimbe, na kuwashwa) na dalili zingine za jumla (kama vile maumivu ya kichwa, maumivu ya misuli, kuhisi kuugua au uchovu), na vilevile kuongezeka au kuzorota kwa hali ya ngozi yako.

## Je, kuna mtu ambaye hawezi kupokea chanjo ya MVA?

Watu ambao hawawezi kupata chanjo ni wale waliopatwa na athari ya ghafla ya mzio inayohatarisha maisha kutokana na dozi ya awali ya chanjo, au kiungo chochote cha chanjo hapo mbeleni. Chanjo ina viwango vichache vya protini ya kuku, benzonase na gentamicin na ciprofloxacin (antibiotiki).

## Je, ni nani anaweza kuwa bora kuchelewesha uchanjaji?

Ikiwa wewe unaugua ukiwa na halijoto ya juu huenda ukahitaji kutathminiwa ili ijulikane kama unaonyesha dalili za mapema za mpox. Ikiwa ugonjwa wako hauhusiani na mpox, bado unaweza kupewa chanjo hiyo. Uwepo wa maambukizi madogo, kama vile homa, hayafai kusababisha uhairishaji wa kutoa chanjo, lakini kwanza zungumza na daktari au muuguzi wako.

## Je, ni nani mwingine anahitaji utunzaji spesheli?

Unapaswa kumwambia daktari au muuguzi ikiwa ulipewa chanjo ya smallpox hapo awali au ikiwa una ugonjwa wa ngozi wa atopiki, kwani hatari ya madhara yanayotokana na chanjo ya MVA inaweza kuwa juu.

Iwapo una VVU (Virusi vya Ukimwi) au una hali nyingine au matibabu yanayopelekea mfumo wa kinga mwilini kudhoofika, huenda chanjo ikakosa kukulinda pia. Hebu hakikisha kwamba daktari au muuguzi wako anajua.

## Utasema nini kuhusu dawa zingine ambazo ninameza?

Mwambie daktari au muuguzi wako iwapo unameza au hapo majuzi ulimeza dawa zingine zozote au iwapo hapo majuzi ulipokea chanjo nyingine yoyote. Katika hali nyingi, unapaswa kuwa sawa kupata chanjo.

Chanjo hiyo inaweza kutolewa kwa usalama kwa watu walioambukizwa virusi vya UKIMWI, wale wanaotumia PreP na wakati uleule kama chanjo nyingine muhimu ikiwa ni pamoja na zile zinazopigana na virusi vya HPV na hepatitis A na hepatitis B.

## Je, MVA hupeanwa kwa njia gani?

Kuna mbinu mbili zinazotumiwa kutoa sindano ya MVA, ikiwezekana katika sehemu ya juu ya mkono. Njia moja hutiwa chini ya ngozi au kwenye misuli (sawa na chanjo nyingine nyingi), ile nyingine hutiwa ndani ya ngozi, kama vile chanjo ya BCG dhidi ya kifua kikuu. Njia zote mbili zina ufanisi sana.

**Kuendesha gari na kutumia Mashine:** Hakuna sababu ya kuamini kwamba chanjo hiyo itaathiri uwezo wako wa kuendesha gari au kutumia mashine. Kuzimia baada ya chanjo ni jambo la kawaida, kwa hiyo unapaswa kungoja dakika 15 baada ya sindano kabla ya kuendesha gari.

## Rekodi ya chanjo ya Mpox

Andika tarehe ya chanjo yako ya mpox hapa chini ili kuhakikisha kuwa hupotezi ulinzi.

Kumbuka, ili ulindwe unahitaji kumaliza kozi kamili ya chanjo:

| Mpox (MVA-BN)<br>Dozi ya chanjo | Tarehe |
|---|---|
| **Dozi ya 1** | |
| **Dozi ya 2**<br>Angalau siku 28 baada ya dozi ya kwanza | |

## Nifanye nini sasa?

Tafadhali muulize muuguzi au daktari wako kwa maelezo zaidi. Chanjo inapatikana kwenye huduma za Specialist Sexual Health (SHSs).

Kwa taarifa zaidi kuhusu mpox na mahali pa kupata chanjo tembelea:

**www.nhs.uk/conditions/mpox/find-a-mpox-vaccination-site**

## Madhara makali

Hali zingine hazijaripotiwa sana kwa watu waliopokea chanjo hiyo. Katika roho ya uwazi, kibandiko cha dawa ya chanjo kinataja hali hizi zote – hata zile zilizoripotiwa kutoka kwa visa vya kipekee – lakini hii haimaanishi kuwa chanjo iliwajibika. Iwapo utapata madhara yoyote, zungumza na daktari wako, mfamasia au muuguzi. Hii inajumuisha madhara yoyote ambayo hayajaorodheshwa kwenye kijikaratasi hiki.

**Kwa kuripoti madhara unaweza kusaidia kutoa habari zaidi juu ya usalama wa chanjo hii.**



NISKANI

Tafadhali ripoti madhara yoyote yanayoshukiwa kupitia tovuti ya Yellow Card Scheme:

**yellowcard.mhra.gov.uk**,

kwa kupakua app ya Yellow Card au kwa kupigia simu Yellow Card scheme kupitia 0800 731 6789 saa 9am – 5pm.

IPATE KWENYE Google Play

Pakua kutoka kwenye App Store

## Utapata habari zaidi kuhusu dawa hii kutoka kwa kibandiko cha vifurushi ambacho daktari au muuguzi anapaswa kukupea.

Kiambatisho kinapatikana pia kwenye tovuti ya Shirika la Dawa la Ulaya: **www.ema.europa/en/medicines/human/EPAR/Imvanex**



© Crown copyright 2025. Product code 2024MPISWA Swahili 1p 20K JAN 2025 (APS). UK Health Security Agency gateway number: 20241029
To order more copies of this leaflet please visit: www.healthpublications.gov.uk or call 0300 123 1002 using product code: 2024MPISWA
Updated 07.02.2025